# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 6

# KISWAHILI PAPER 3 ANSWERS

SEHEMU A (Alama 20 )

SWALI LA LAZIMA

1(a)

(i) Msemaji ni Bili

(ii) Wasemewa ni Meya,Diwani I na Diwani II.

(iii)Wako ofisini mwa Meya.

waliokuwa wanagoma huku akiwatahadharisha wawe waangalifu kwani wageni walikuwa wanatarajiwa wasipate picha mbaya ya Cheneo. (Tuza -4x1=4)

(b) Waathiriwa wa virungu walifanya fafuatayo ili kujikwamua kwa hilo lililowakumba:-

(i)Wafantyakazi walienda kumwona Meya.

(ii)Wafanyakazi kugoma na kuacha toka mjini na kotekote.

(iv)Viongozi wa wafanyakazi walikutana na Meya kuwalisha lalama zao k.m.Akina Bekena Tatu.

(v)Siki alimshauri Diwani III kutumia nafasi yake kumwelezea Meya matatizo ya wanacheneo.

(vi)Waliandamana k.m wafanyakazi wa uwanja wa ndege uk 76.

(vii)Askari walimwondoa Meya madarakani kupitia mapinduzi. (zozote 7x2=14)

SEHEMU B (Alama 20 )

RIWAYA

2.(a) Muktadha Uk.88

(i)Msemaji –Mtemi Nasaba Bora.

(ii)Msemewa ni Askari.

(iii) Wako kwenye majengo ya seli.

pale kuliko kuwa askari ndipo akawauliza wawafanyie kazi wale mahabusu.(Amani na Imani) (1x4=4)

(b)Maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili ni:-

(i)Dhuluma –kuwapiga na kuwaweka katika seli kwa makosa wasiofanya-kuna kitoto Uhuru.

(ii)Ukatili wa ukosefu wa utu-matusi,kipigo na tuhuma za uongo.

(iii)Unyonyasaji wa wanyonge-kupagazwa kitoto na kisha kusingiza mauaji.(zozote 2x1=2)

(c)Wengine walioathiriwa na maudhui hayo ni:-

(i) Bob DJ kufungwa jela kwa kusingiziwa kaiba.

(ii) Yusuf kafungwa jela kwa kutuhumwa kuwa ndiye aliyemuuwa babke. wazalendo.

(iv)Mamke Imani kwa kuchomewa nyumba na kuuawe huku shamba lake likinyang'anywa.

(v)Amani anadhulumiwa mswada wake unapoibiwa na Mafisifu.

(vi) Kitoto Uhuru kinadhulumiwa katika zahanati;wale wauguzi wanapokataa kukishughulikia siku kuu ya wazalendo-kisha kinaaga.

(vii) Mwanafunzi anayepingwa na Fao na kisha kupuuzwa yeye na mwanawe na hata kukatiza masomo yake.

(viii) Wanasokomoko kulazimishwa kutoa pesa za kumsomesha mwanawe Mtemi kule Urusi ni unyanyasaji wa aina yake. *mtahiniwa aweze kuongezea (zozote 6x2=12

3.Matumizi ya mbinu ya

(a) Sadfa:ni matukio mawili kutokea wakati mmoja bila kupangwa.

(i) Ni sadfa kuwa Bw.Majisifu analala chumba tofauti na mkewe ili asizae tena lakini siku wanaolala pamoja,mkewe anapata mimba na hatimaye anajifungua watoto viwete.

(ii) Ni sadfa kuwa ng'ombe anaitafunatafuna kaptura ya DJ siku ambayo Amani amefika pale karibu na shati lake na kumwondolea aibu.

(iii) Ni sadfa kuwa Imani na Amani walifika Sokomoko wakati ambapo Bw.Nasaba Bora na mwalimu Majisifu wanataka wafanyakazi hivyo basi kupata kazi hizo.

(iv) Ni sadfa kuwa Imani anapoamua kujitia kitanzi anaenda kupanga hivyo katika Ziwa mawewa lakini anapofika huko akitaka kujitosa ziwani anaskia sauti nzuri inayofanfanya achilie kujitupa na ndivyo anavyokutana na Amani.

(v) Asklari wana redio inayotangaza sifa za chwechwe wakati dadake Imani yuko katika seli

(vi) Ni sadfa kuwa Amani na Imani wanakutana kisadfa,wamedhulumiwa na mtu mmoja aliyewanyang'anya mali yao na kusababisha vifo vya jamaa zao njiani Mtemi Nasaba Bora.

(vii) Azma ya madhubuti/nasadifiana na ile ya Amani kwani wote wanapania kurejesha haki katika Tomoko

(viii) Ni sadfa kuwa Amani na Yusufu wanajipata gerezani wakati mmoja ndiposa Amani anaelezwa jinsi mali ya Nasaba yake ilivyonyakuliwa.(uk 117)

(ix) Imani anaitwa na Dora baada ya kuisoma barua ya Amani na anawacha,jambo lililomfanya mwalimu Majisifu aipate.(uk 142)

(x) Amani alipoomba kitabu cha kusoma akiwa kwa Majisifu analetewa kile chake cha kidagaa kimemwozea ambacho kiliimbwa kikiwa mswada.

(xi) Amani Anapoitwa na Zuhura usiku katika chumba chake cha kulala,na Nasaba Bora anarejea usiku na kuwakuta.Nasaba Bora anaamini kuwa walikuwa wakifanya mapenzi. (zozote 10x1=10)

(b) Matumizi ya barua.

(i) Kuma barua kutoka kwa Ben Bella mchumbaye Mashaka,akimweleza ukatili wa Nasaba Bora aliyempachika Lowela mimba na kumpeleka mbali.Hatimaye Ben anaomba kukatiza uhusiano wake na Mashaka.Ndio chanzo cha Mashaka kuwa punguani baada ya kushindwa kuendelea na masomo.

(ii) Kuna barua kwa Madhubuti,mwanawe Mtemi Nasaba Bora akimwambia kuwa angerudi mwisho wa mwezi lakini hakutaka kusaidiwa kupata kazi bali alitaka ajisimamie,kuonyesha mapinduzi na mwanzo wa uasi.

(iii) Kuna barua kutoka kwa chuo kikuu cha Mkokotoni kumwendea mwalimu Majisifu ili aende chuoni kutoa mhadhara kuhusu riwaya ya Kidagaa Kimemwozea na masuala mengine ya lugha na fasihi ya Kiswahili na utamaduni.

(iv) Kuna barua kutoka kwa Lowela Maozi kumwonya Mtemi Nasaba Bora kuwa siri ya mahaba yao angeilipua ikiwa asingewaachukilia huru Imani na Amani; yaonyesha kujali kwa Lowela na kutetea kwake vijana hawa ambao anajua kuwa hawana hatia.

(v) Kuna barua kutoka kwa Amani hadi kwa Imani baada ya ujanja wa Majisifu kujulikana kuhusika na msuada wa Kidagaa Kimemwozea.Amani alikuwa akiugua kiasi cha kutoweza kusoma (uk 142) Barua hii inatoa pia katika mbinu rejeshi habari kwa Imani kuhusu maisha yake ya awali ambayo Amani hakuweza kumfichulia walipopatana mara ya kwanza.(zozote 5x2=10)

SEHEMU C (Alama 20 )

HADITHI FUPI

4.(a) Muktadha (uk 29)

(i) Msemaji ni mwandishi/msimulizi/Fikirini au fikira za Fikirini.

(ii) Anaeleza masaibu yaliyompta Fikirini mikononi mwa wazungu weusi-Fiona na Bob huku akikumbuka kifo cha mamye.

(iii) Wako nyumbani mwa Fiona.

(iv) Wakati akiporwa na kutishiwa kuuawa na aliowadhania kuwa ndugu zake weusi kule marekani. (tuza 4x1=4)

(b)Mbinu mbili za lugha katika dondoo hili ni: (i) Methali –siku ya nyani kufa mti yote huteteleza.

(ii) Jazanda –nyani ilio na maana ya mtu kimuktadha. (tuza 2x2=4)

(c)(i) Mzungumzaji aliulizwa maswali ya kudunisha k.m. mbona mnapigana huko kwenu.

(ii)Aliachwa na basi kenye steji kwa ajili ya weusi wake kudhaniwa jambazi.

(iii)Waliadhiri chuoni waliwatuza alama chache wakilinganishwa na wazungu.

(iv)Alipigwa na kutishiwa kupigwa bunduki na kuporwa mali yake yote.

(vi) Alibaguliwa mahakamani kwa kutozwa faini kubwa kwa makossa ambayo wazungu hata hawakushtakiwa k.m. kusahau kufunga zipu na kuvuka barabara taa nyekundu zikiwa zinawaka.

(vii) Alituhumiwa kuwa mwizi madukani na kwa hivyo kufuatwa na wahudumu wa hapo kila alipopitia. *mtahiniwa aweze kuongezea. (zozote 6x2=12)

5.Vijana wanakumbumwa na chanagamotro kadha katika maisha.Dhihirisha kwa mujibu Kanda la Usufu. Jawabu Baadhi ya changamoto zinazojitokeza ni:

(i)Utovu wa nidhamu kwa vijana kushiriki mahusiano ya kimapenzi wakiwa bado shuleni.

(ii)Matatizo ya ulezi wa mimba huku wataka wasome.

(iii)Kujiingiza katika ndoa za mapema bila mpango na hivyo hazifaulu.masomo kwanza.

(v)Kulazimika kukatiza masomo na huku hana la kufanya muhimu k.v Sela.

(vi) Kukosa subira, wangesubiri hadi muda unaofaa suala la mapenzi na ndoa pengine mkasa unawaowakumba haungewapata.

(vii) Ni changamoto mwanafunzi kulea mtoto huku yuaenda shule afaulu k.v Sela tuambiwa alirudi shule laikni haijulikani kama alifaulu.

(viii) Vijana hawako tayari kwa majukumu ya vitendo vyao. K.m wanamuacha mtoto kisha baadaye wanarudi kumuiba usiku.

(ix) Mara mingi vijana hawawezi matokeo ya vitendo vyao k.m Sela kuithamini barua iliomletea shida –mimba pia uamuzi wa kwenda kumchukuwa mwanao usiku huku mvua inanyesha – mwisho kifo.

(x) Wavulana wanaowaringa wasichana kwa jiusi hii hata nao hawafanikiwi –k.m Masazu haelekei kufaulu na amenda mjini kuvuna mkonge.

(xi) Vijan hawawajibikii uhusiano wao na ndio maana Sela anakua mjamzito.

*Mtahini:Akadirie (zozote 20x2=20)

SEHEMU D (Alama 20 )

FASIHI SIMULIZI

6.(a)

(i) Ni aina ya Sanaa ambayo wahusika huiga vitendo vya watu mbalimbali kutoka kwa jamii na viumbe ili kupasha ujumbe.

(ii) Ni masimulizi ambayo yanaombatana na vitendo au matendo Fulani na kufanywa mbele ya hadhira au watazamaji jukwaani. (yoyote 1x2=2)Aina nne za maigizo:

(i) Michezo jukwaani

(iii)Vichekesho.

(iv)Ngonjera.

(v)Miviga.

(vi)Ngomezi.

(vii)Utambaji wa hadithi.

(viii)Unyago.

(ix)Michezo ya watoto. (zozote 4x1=4)

(c)Sifa za maigizo:

(i)Huwa na vitendo vingi tofauti.

ii)Hujenga taswira kwa ufundi wa hali ja juu kwa kutumia tamathali,semi na mafumbo.

(iii)Hutumia vinyago na vifaa maalum kufanikisha ujumbe.

(iv) Sharti kuwe na utendaji/uigizaji.

(v) Hutegemea sauti na maleba ingawa mchezo bubu hautumii sauti/maneno.

(vi) Huambatana na ngoma na nyimbo wakati mwingine.

(vii) Wahusika huingia mambo yanayopatikana na jiusi yanavyoonekana katika jamii.

(viii) Hutegemea matukio ya wakati huo. (zozote 4x1=4)

d) Majukumu ya maigizo katika jamii.

(i) Kuelimisha,kuadilisha na kufahamisha juu ya mambo mbalimbali yanayowahusu wanajamii.

(ii)Hukuza msamiati na matumizi ya lugha.

(iii) Hufufua,hudumisha na kuendeleza utamaduni.

(iv) Huimarisha vipawa vya waigizaji wanapojihusisha na utendaji wa maigizo.

(vi) Hutumiwa kukeji mtu/watu au jambo fulani ambalo linachukukiza katika jamii. hisia za watu.

(viii) Kuendeleza jamii ili kikazi kifacho kisisahau mabo ya jamii husika.

(ix) Hutabiri mambo yafayo na pia kutoa suluhusho kwa matatizo yanayokumba jamii.

(e) Njia TANO za kuendeleza:

kuzungumzia na miongoni vijana wa asasi mbalimabli za elimu

(ii) Kwa kupanga michuano baina ya shule mbalimbali ambapo aina mbalimbali za fasihi simulizi zinawasiliana na wanafunzi k.m mashindano ya maigizo.

(iii) Kuwezesha vyombo vya habari kama redio kuwasilisha aina tofauti za fasihi simulizi

k.m nyimbo,ngano na vitanza ndimi ambazo huelimisha wanafunzi.

(iv) Kwa kusisitiza usomajin wa fasihi simulizi katika silabasi n ahata kutahini ili wanafunzi waweze bayana vipengele vya kimsingi vya fasihi simulizi.

(v) Kwa kuwapo motisha waandishi wa vitabu vya fasihi waweze kuandika ili watu waweze kusoma,kujua na kuweza kuwasilisha aina mbalimbali za fasihi simulizi.

(vi) Kwa huwezesha miradi ya utafiti wa fasihi simulizi ili aina mbalimbali za Fasihi simulizi Ziweze kuvumbuka na kueleweka.

(vii) Kwa kupanga vikao ambapo walimu wa Fasihi simulizi wanaweza kushauiriana na kuweza kufunza wanafunzi maarifa maarifa zaidi waliyopata. (Za kwanza 5x1=5)

SEHEMU E (Alama 20 )

USHAIRI

7.(a) Ajira ya watoto/watoto kutumikishwa/ukiukaji wa haki za watoto. (alama 1)

ukiukali wa haki za watoto. Alama 1 (1x1=1)

(b) Muundo/sura.

(i)Shairi hili lina beti 8.

(ii)Kila mshoroor una mishororo mine (tarbia)kwa hivyo ni mathnawi.

(iv)Kila mshororo una mizani 16.

(v)Vina vya shairi hili vinabadilika badilika toka ubeti mmoja hadi mwingine k.m ubeti wa kwanza.

Sa-vi

Sa-vi

Sa-vi

(c) Watoto hutumikishwa katika manyumbani kwama vijakazi.

(ii) Kwenye mitaa kwa ufuska/Malaya.

(iv) Katika viwandani kwa kazi za sulubu k.v kubeba magunia. (zozote 2x1=2)

kibwagizo kwa kusema komeni tena komeni. (1x2=2)

(e) Dhamira ya mshairi ni kuwa watoto wasitumishwe na kudhulumiwa na badala yake wapelekwe shuleni wasome kwa sababu taifa linawasubiri baadaye waliendeleze. Haki za watoto zisingatiwe vilivyo. (1x1=2)

(f) Madukani hubebeshwa majina na kwa hivyo kuharibu afya yao.Wapewe muda wa kujiendeleza kwa kukoma kuwapa kazi.

(g)(i)Mtunzi ameboronga lugha k.m komeni,tena komeni watoto kuwaajiri badala ya komeni kuwajiri watoto.

(ii)Ametumia inkisari k.v Damuyo badala ya damu yake,takutia-itakutia n.k

(iii)Tabdila k.m wajuuza badala ya wajiuza. (zozote 2x1=2)

(h)(ii)Kusombeshwa –Bebeshwa/fanyishwa.